

Serikali kuendelea kuwezesha mbegu za malisho

Na Amina Omari, Tanga

SERIKALI imesema kuwa itaendelea kuziwezesha Taasisi zake za utafiti wa mifugo ili ziweze kuendelea kutafiti mbegu bora za malisho na kuwasaidia wafugaji mifugo yao izalishe mazao yenye ubora.

Ahadi hiyo imetolewa na Mkurugenzi wa Utafiti, Mafunzo na Ugani kutoka wizara ya Mifugo na Uvuvi,

Dk Angello Mwilawa wakati wa ziara ya mafunzo kwa wafugaji kutoka mikoa mbalimbali, Taasisi ya Mifugo ya TALIRI kituo cha Tanga.

Alisema ni lengo la serikali kuhakikisha wafugaji wake wanazalisha bidhaa bora kwa kuzingatia mazingira.

Dk Mwilawa alisema kuwa serikali inataka kuhakikisha wafugaji wanakuwa na mifugo michache

ambayo inafugwa katika eneo dogo yenye kuzalisha kwa tija.

Kwa upande wake Msi-mamizi Mkuu wa Mradi wa malisho ambayo ni rafiki wa mazingira Dk An Notenbaert alisema kuwa TALIRI kwa kushirikiana na Shirika la utafiti wa malisho Afrika SIAT waliweza kuendesha Mradi huo wa utafiti wa malisho kwa kipindi cha miaka minne.

Alisema kuwa malisho

haya yameonyesha tija kubwa kwa wafugaji kwani wameweza kupata mazao yenye ubora lakini mifugo imeweza kuzalisha kwa wingi tofauti na hapo awali.

Alisema kuwa wafugaji wamekuwa tayari kujifunza Teknolojia hii mpya kwani tukiweza kuanza na wafugaji 36 pekee lakini sasa mbegu hiyo imeweza kusambaa kwa wafugaji wengi zaidi katika kipindi kifupi.

Wafugaji walisema

wanaushukuru mradi huo kwa kuwasaidia kupata malisho ya uhakika hata katika Yale maeneo yenye ukame wameweza kuzalisha malisho hayo na mifugo yao imeonyesha tija kubwa.

Nae Mfugaji kutoka Muheza, Ester Makenye alisema kuwa hapo awali waliletewa aina mbalimbali za nyasi kwa ajili ya mifugo lakini mbegu aina ya Kobra imeonyesha matokeo mazuri na ya haraka.

Mfugaji kutoka Njombe Susan Chagawa aliiomba wizara ya mifugo kuendelea kufanya tafiti kwa malisho asilia ili kuona namna ambavyo wataweza kuyaboresha ili nayo yaweze kutoa matokeo bora.

Mradi wa malisho ambayo ni rafiki wa mazingira umetekelezwa katika wilaya za Rungwe, Njombe, Mufindi, Muheza, Mkinga na Hai ambapo unatarajiwa kufikia ukomo wake mwaka huu.

Habari leo uk. 20, Tarehe

12/06/2021

Kwa Ufupi

Wafugaji watishia shamba la miti



Mvomero. Baadhi ya wafugaji waliopo jirani na shamba la miti Mtibwa sehemu ya Pagale, Wilaya Mvomero wanatuhumiwa kuvamia kambi, kuharibu na kupora ng'ombe walio-kamatwa kwa kuingia kwenye hifadhi hiyo.

Hayo yamebainika jana wakati Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) ilipotembelea shamba hilo linalomilikiwa na Wakala wa Hudumu za Misitu (TFS) ili kufanya ukaguzi wa shughuli zilizotekelezwa kwa kutumia fedha za ruzuku ya zaidi ya Sh500 milioni iliyotolewa na TaFF kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2021.

Mwananchi Uk.24

Tarehe 12/06/2021